

Maelezo ya Utafiti

Kupata Makazi: Wakimbizi wakiendesha njia zao

Vita, machafuko ya kisiasa, na, mabadiliko ya hali ya hewa yamechangia kuongezeka kwa hesabu ya wakimbizi kote duniani. Katika jamhuri ya kidemokrasia ya Congo, vita vinavyoendelea na migogoro imesababisha wakimbizi kutoroka kutoka nchi zao katika hali ngumu sana. Wengi wameishi kwa muda katika kambi za wakimbizi. Wengine wamepata makazi mapya katika nchi ya marekani pasi na matayarisho ya kutosha. Tunaandika kitabu kuhusu familia za wakimbizi wakongo ambao wanajaribu kuzoea maisha marekani. Blair Sackett, mwanafunzi aliyehitimu, aliweza kujua tano kati ya hizi familia walipowasili mwaka wa elfu mbili kumi na tano, akiwatembelea na kuwahoji, akiandika kuhusu changamoto na mafanikio waliyoyapata katika miaka tano iliyopita. Sasa, ili kumaliza, tunafanya mahojiano ya simu na kwenye mtandao wa zoom na familia zingine za wakimbizi wakongo, haswa wale wanaoishi katika eneo la Philadelphia. Mahojiano ni katika lugha ya Kiswahili ama kiingereza. Blair na wanafunzi wengine watatu wa shahada ya chini wanaosaidia katika utafiti Maria Apiyo Odongo, Mirriam Chemutai, na Frida Aloo, wanafanya mahojiano. Kwa wakimbizi, tunapeana kadi ya zawadi kama shukrani kwa kutusaidia.

Tunajaribu kuelewa jinsi watu wageni hupata kazi, usimamizi wa fedha, ushirikiano wao na ofisi za serikali na uzoefu wao wa shule za marekani. Pia tunazungumza na wafanyikazi wa misaada na wale wa kujitolea, ambao wamefanya kazi na familia hizi za wakimbizi. Kila kitu ni siri, ikiwemo majina kamili ya watu ambao tumewahoji ili kuhakikisha kutokujulikana.

Baada ya kumaliza utafiti huu, tutaandika kitabu kuhusu maisha wa wakimbizi wakongo ambao wamepata makaazi mapya huku, na mambo ambayo tumejifunza kutokana na kuongea na wakimbizi na wale ambao wanawasaidia. Kitabu hicho kitachapishwa na chuo kikuu cha California. Matumaini yetu ni kuwa itaimarisha kuelewa, sio tu kwa wanafunzi katika vyuo vikuu bali kwa wafanyikazi wa kujitolea wa makanisa, wafanyikazi wa misaada, na kila mtu ambaye anasaidia wakimbizi katika mapito hata wanapofuatilia ndoto zao za marekani.

Iwapo una maswali yoyote kuhusu utafiti huu tafadhali wasiliana na:

Professor Annette Lareau (alareau@sas.upenn.edu)

Blair Sackett (bsackett@sas.upenn.edu)